JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA WA KIDATO CHA NNE ULIOFANYIKA NOVEMBA, 2024

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MTENDAJI**
**TAREHE: 23 JANUARI 2025**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **164** uliofanyika tarehe **22 Januari**, **2025**, Baraza la Mitihani la Tanzania liliidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) uliofanyika mwezi Novemba, 2024.

## 2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

### (a) Watahiniwa Wote

Jumla ya watahiniwa **557,796** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne wakiwemo Wasichana **296,051** (**53.08%**) na Wavulana **261,745** (**46.92%**). Kati ya watahiniwa **557,796** waliosajiliwa, watahiniwa wa Shule walikuwa **529,329** na watahiniwa wa Kujitegemea walikuwa **28,467**.

### (b) Watahiniwa wa Shule

Kati ya watahiniwa **529,329** wa Shule waliosajiliwa, watahiniwa **517,460** sawa na asilimia **97.76** walifanya mtihani ambapo Wasichana walikuwa **271,918** sawa na asilimia **97.54** ya Wasichana wote huku Wavulana wakiwa **245,542** sawa na asilimia **98.00** ya Wavulana wote. Watahiniwa **11,869** sawa na asilimia **2.24** hawakufanya Mtihani.

### (c) Watahiniwa wa Kujitegemea

Kati ya watahiniwa **28,467** wa Kujitegemea waliosajiliwa, watahiniwa **25,151** sawa na asilimia **88.35** walifanya Mtihani na watahiniwa **3,316** sawa na asilimia **11.65** hawakufanya Mtihani.

## 3.0 MATOKEO

### 3.1 Ufaulu wa Ujumla

#### (a) Watahiniwa wa Shule

Jumla ya watahiniwa wa Shule **477,262** kati ya **516,695** wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia **92.37** wamefaulu ambapo wamepata Madaraja ya **I**, **II**, **III** na **IV**. Mwaka 2023 Watahiniwa waliofaulu walikuwa **471,427** sawa na asilimia **89.36**. Hivyo, ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **3.01**.

Kati ya watahiniwa **477,262** waliofaulu, Wasichana ni **249,078** sawa na asilimia **91.72** ya Wasichana wote wenye matokeo na Wavulana ni **228,184** sawa na asilimia **93.08** ya Wavulana wote wenye matokeo.

**(b) Watahiniwa wa Kujitegemea**

Watahiniwa wa Kujitegemea waliofaulu mtihani ni **15,703** sawa na asilimia **62.51**. Mwaka 2023 Watahiniwa wa Kujitegemea **13,396** sawa na asilimia **52.44** walifaulu mtihani huo. Hivyo, ufaulu wa Watahiniwa wa Kujitegemea **umepanda** kwa asilimia **10.07** ikilinganishwa na mwaka 2023.

Mchanganuo wa ufaulu wa Jumla katika Mtihani wa CSEE 2024 umeainishwa katika **Jedwali Na.1**

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Jumla katika Mtihani wa CSEE 2024**

| Aina ya Watahiniwa | Mwaka | Jinsi | Wenye Matokeo | Waliofaulu | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % |
| Wa Kujitegemea | 2023 | Wasichana | 15,359 | 7,745 | 50.43 |
| | | Wavulana | 10,184 | 5,651 | 55.49 |
| | | Jumla | 25,543 | 13,396 | 52.44 |
| | 2024 | Wasichana | 15,478 | 9,605 | 62.06 |
| | | Wavulana | 9,642 | 6,098 | 63.24 |
| | | Jumla | 25,120 | 15,703 | 62.51 |
| Wa Shule | 2023 | Wasichana | 283,911 | 250,147 | 88.11 |
| | | Wavulana | 243,665 | 221,280 | 90.81 |
| | | Jumla | 527,576 | 471,427 | 89.36 |
| | 2024 | Wasichana | 271,555 | 249,078 | 91.72 |
| | | Wavulana | 245,140 | 228,184 | 93.08 |
| | | Jumla | 516,695 | 477,262 | 92.37 |

## 3.2 Ubora wa Ufaulu

Watahiniwa wa Shule waliopata ubora wa ufaulu katika Madaraja ya **I - III** ni **221,953** sawa na asilimia **42.96**. Mwaka 2023 watahiniwa waliopata ufaulu wa Madaraja ya **I - III** walikuwa **197,426** sawa na asilimia **37.42**. Hivyo, ubora wa ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **5.54** ikilinganishwa na mwaka 2023.

Ubora wa ufaulu wa Madaraja ya **I - III** ni mzuri zaidi kwa Wavulana ikilinganishwa na Wasichana ambapo Wavulana ni **119,869** sawa na

asilimia **48.90** ya Wavulana wote wenye matokeo na Wasichana ni **102,084** sawa na asilimia **37.59** ya Wasichana wote wenye matokeo. Mchanganuo wa ufaulu katika Madaraja mbalimbali umeainishwa katika **Jedwali Na.2**.

**Jedwali Na.2: Ufaulu wa Jumla Kimadaraja kwa Watahiniwa wa Shule**

| Daraja | Mwaka | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| I | 2023 | 24,717 | 10.14 | 17,731 | 6.25 | 42,448 | 8.05 |
| | 2024 | 26,308 | 10.73 | 19,530 | 7.19 | 45,838 | 8.87 |
| II | 2023 | 39,804 | 16.34 | 31,451 | 11.08 | 71,255 | 13.51 |
| | 2024 | 41,863 | 17.08 | 34,000 | 12.52 | 75,863 | 14.68 |
| III | 2023 | 43,847 | 17.99 | 39,876 | 14.05 | 83,723 | 15.87 |
| | 2024 | 51,698 | 21.09 | 48,554 | 17.88 | 100,252 | 19.40 |
| I - III | 2023 | 108,368 | 44.47 | 89,058 | 31.37 | 197,426 | 37.42 |
| | 2024 | 119,869 | 48.90 | 102,084 | 37.59 | 221,953 | 42.96 |
| IV | 2023 | 112,912 | 46.34 | 161,089 | 56.74 | 274,001 | 51.94 |
| | 2024 | 108,315 | 44.18 | 146,994 | 54.13 | 255,309 | 49.41 |
| I - IV | 2023 | 221,280 | 90.81 | 250,147 | 88.11 | 471,427 | 89.36 |
| | 2024 | 228,184 | 93.08 | 249,078 | 91.72 | 477,262 | 92.37 |
| 0 | 2023 | 22,385 | 9.19 | 33,764 | 11.89 | 56,149 | 10.64 |
| | 2024 | 16,956 | 6.92 | 22,477 | 8.28 | 39,433 | 7.63 |

### 3.3 Ufaulu wa Shule katika Makundi ya Umahiri

Kati ya shule zote **5,563** zenye matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne 2024, shule **5,552** (**99.80%**) zimepata wastani wa Daraja la **A-D** ikilinganishwa na shule **5,334** (**99.83%**) zilizopata wastani wa Madaraja hayo mwaka 2023. Aidha, shule zilizopata wastani wa Daraja la **A-C zimeongezeka** kwa asilimia **7.45** kutoka idadi ya shule **1,997** (**37.38%**) mwaka 2023 hadi kufikia idadi ya shule **2,494** (**44.83%**) mwaka 2024. Mchanganuo zaidi umebainishwa katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2024 ikilinganishwa na Mwaka 2023**

| Daraja | 2024 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % |
| A | 110 | 1.98 | 97 | 1.82 |
| B | 593 | 10.66 | 565 | 10.57 |
| C | 1,791 | 32.19 | 1,335 | 24.99 |
| D | 3,058 | 54.97 | 3,337 | 62.46 |
| F | 11 | 0.20 | 9 | 0.17 |

## 3.4 Ufaulu wa Watahiniwa Kimasomo

### 3.4.1 Masomo ya Sayansi Jamii

Watahiniwa waliofaulu masomo ya **Civics**, **History** na **Geography** ni kati ya asilimia **70.34** hadi **73.36**. Masomo yote ya Sayansi Jamii **yameongezeka** ufaulu kati ya asilimia **2.51** hadi **10.16** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2023. Aidha, somo la **History** limeongezeka ufaulu kwa asilimia **10.16** likifuatiwa na somo la **Geography** lililoongezeka ufaulu kwa asilimia **7.59**. Watahiniwa waliopata ubora wa ufaulu kati ya gredi **A** hadi **C** katika masomo ya Sayansi Jamii ni kati ya asilimia **31.69** hadi **39.54** ambapo somo la History lina asilimia kubwa (**39.54**) ya watahiniwa waliopata gredi **A**, **B** na **C**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Sayansi Jamii umeoneshwa katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Jamii**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Civics | 2023 | 527,671 | 1.71 | 6.26 | 30.91 | 67.83 | 32.17 |
| | 2024 | 516,610 | 1.14 | 4.96 | 31.69 | 70.34 | 29.66 |
| History | 2023 | 517,051 | 2.18 | 7.01 | 30.48 | 63.20 | 36.80 |
| | 2024 | 504,936 | 2.88 | 9.60 | 39.54 | 73.36 | 26.64 |
| Geography | 2023 | 526,789 | 1.27 | 5.26 | 30.33 | 64.32 | 35.68 |
| | 2024 | 515,394 | 2.84 | 9.06 | 37.10 | 71.91 | 28.09 |

### 3.4.2 Masomo ya Lugha

Watahiniwa wengi wamefaulu somo la **Kiswahili** ambao ni asilimia **97.43**. Watahiniwa waliofaulu masomo ya **English Language**, **French Language**, **Literature in English** na **Chinese Language** ni kati ya asilimia **75.93** hadi **86.23**. Aidha, somo la **Arabic Language** ufaulu unaendelea kuimarika kutoka asilimia **26.83** mwaka 2023 hadi **33.86** mwaka 2024.

Watahiniwa waliopata ubora wa ufaulu wa gredi **A** hadi **C** ni asilimia **71.53** katika somo la **Kiswahili**, na katika masomo ya **English Language**, **Literature in English** na **Chinese Language** ni kati ya asilimia **41.21** hadi **52.93**. Aidha, watahiniwa waliopata gredi za ubora katika masomo ya **French Language** na **Arabic Language** ni wachache ambao ni kati ya asilimia **13.34** na **26.10**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Lugha umeoneshwa katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Lugha**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | 2023 | 527,708 | 4.25 | 18.87 | 74.39 | 96.80 | 3.20 |
| | 2024 | 516,610 | 1.17 | 8.44 | 71.53 | 97.43 | 2.57 |
| English Language | 2023 | 527,672 | 1.34 | 5.41 | 27.49 | 69.09 | 30.91 |
| | 2024 | 516,610 | 3.40 | 10.16 | 41.21 | 76.09 | 23.91 |
| French Language | 2023 | 2,338 | 0.81 | 3.64 | 27.33 | 79.56 | 20.44 |
| | 2024 | 2,310 | 1.43 | 4.72 | 26.10 | 75.93 | 24.07 |
| Literature in English | 2023 | 114,727 | 0.87 | 5.90 | 42.40 | 79.34 | 20.66 |
| | 2024 | 123,902 | 2.50 | 10.59 | 52.93 | 86.23 | 13.77 |
| Arabic Language | 2023 | 14,609 | 0.64 | 1.86 | 8.88 | 26.83 | 73.17 |
| | 2024 | 12,955 | 0.66 | 2.66 | 13.34 | 33.86 | 66.14 |
| Chinese Language | 2023 | 440 | 6.14 | 19.09 | 54.09 | 91.36 | 8.64 |
| | 2024 | 509 | 5.89 | 15.13 | 41.45 | 79.17 | 20.83 |

### 3.4.3 Masomo ya Sayansi Asilia, Hisabati na Teknolojia

Ufaulu wa masomo ya **Chemistry**, **Agriculture**, **Engineering Science**, **Information and Computer Studies**, **Additional Mathematics** na **Food and Human Nutrition** ni kati ya asilimia **93.00** hadi asilimia **100** ambapo ufaulu wa juu upo katika somo la **Food and Human Nutrition** ambalo watahiniwa wote waliofanya somo hilo wamefaulu likifuatiwa na somo la **Chemistry** asilimia **96.36**. Aidha, watahiniwa waliofaulu masomo ya **Physics** na **Biology** ni kati ya asilimia **73.98** na **74.15**. Somo la **Basic Mathematics** lina ufaulu ulio chini ya wastani ambao ni asilimia **25.35**. Ufaulu wa masomo yote ya **Sayansi Asilia na Teknolojia** umepanda kati ya asilimia **0.22** hadi **8.07**. Aidha, ufaulu wa somo la **Basic Mathematics** umeshuka kidogo kwa asilimia **0.07** na katika somo la **Additional Mathematics** umeshuka kwa asilimia **2.70** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2023.

Ubora wa ufaulu ni mzuri katika masomo ya **Chemistry**, **Agriculture**, **Engineering Science**, **Information and Computer Studies**, **Additional Mathematics** na **Food and Human Nutrition** ambapo kati ya asilimia **64.52** hadi **97.88** ya watahiniwa wamepata ufaulu wa gredi **A** hadi **C**. Somo la **Biology** limeimarika ubora wa ufaulu kutoka asilimia **35.36** mwaka 2023 hadi **40.04** mwaka 2024. Aidha, ubora wa ufaulu umeshuka kidogo katika somo la **Basic Mathematics** kwa asilimia **1.04**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Sayansi Asilia, Hisabati na Teknolojia umeoneshwa katika **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Asilia, Hisabati na Teknolojia**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Physics | 2023 | 121,644 | 1.03 | 5.03 | 32.82 | 71.85 | 28.15 |
| | 2024 | 121,895 | 1.65 | 5.84 | 32.59 | 73.98 | 26.02 |
| Chemistry | 2023 | 162,026 | 10.67 | 30.01 | 77.82 | 96.14 | 3.86 |
| | 2024 | 164,773 | 5.83 | 21.31 | 74.95 | 96.36 | 3.64 |
| Biology | 2023 | 527,574 | 2.24 | 8.05 | 35.36 | 70.09 | 29.91 |
| | 2024 | 516,637 | 4.54 | 11.74 | 40.04 | 74.15 | 25.85 |
| Agriculture | 2023 | 6,820 | 1.36 | 5.63 | 49.46 | 88.49 | 11.51 |

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2024 | 8,111 | 1.44 | 8.37 | 64.52 | 95.01 | 4.99 |
| Engineering Science | 2023 | 1,573 | 9.35 | 22.95 | 58.55 | 84.93 | 15.07 |
| | 2024 | 1,643 | 15.40 | 38.59 | 77.48 | 93.00 | 7.00 |
| Information and Computer Studies | 2023 | 3,517 | 8.56 | 26.16 | 70.15 | 89.88 | 10.12 |
| | 2024 | 4,292 | 20.76 | 40.75 | 79.12 | 93.50 | 6.50 |
| Basic Mathematics | 2023 | 527,608 | 1.84 | 4.11 | 12.75 | 25.42 | 74.58 |
| | 2024 | 516,520 | 1.99 | 3.91 | 11.71 | 25.35 | 74.65 |
| Additional Mathematics | 2023 | 417 | 15.83 | 35.01 | 78.90 | 97.84 | 2.16 |
| | 2024 | 370 | 19.73 | 36.49 | 72.97 | 95.14 | 4.86 |
| Food and Human Nutrition | 2023 | 2,241 | 13.43 | 58.50 | 99.38 | 100 | 0.00 |
| | 2024 | 2,359 | 6.49 | 38.91 | 97.88 | 100 | 0.00 |

### 3.4.4 Masomo ya Biashara

Watahiniwa waliofaulu somo la **Commerce** ni asilimia **89.17** na waliofaulu somo la **Book-Keeping** ni asilimia **88.27**. Aidha, ufaulu wa somo la **Commerce** umeongezeka kwa asilimia **8.15** na ufaulu wa somo la **Book-Keeping** umeongezeka kwa asilimia **9.65**.

Watahiniwa waliopata ubora wa ufaulu wa gredi **A** hadi **C** katika somo la **Commerce** ni asilimia **50.58** na katika somo la **Book-Keeping** ni asilimia **54.98**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Biashara umeoneshwa katika **Jedwali Na. 7**.

**Jedwali Na. 7: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Biashara**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Commerce | 2023 | 13,544 | 0.75 | 4.70 | 37.81 | 81.02 | 18.98 |
| | 2024 | 13,018 | 1.44 | 7.34 | 50.58 | 89.17 | 10.83 |
| Book-Keeping | 2023 | 13,203 | 1.67 | 6.75 | 38.83 | 78.62 | 21.38 |
| | 2024 | 12,589 | 1.78 | 9.47 | 54.98 | 88.27 | 11.73 |

### 3.4.5 Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Ufaulu wa somo la **Fine Art**, **Music, Physical Education** na **Theatre Arts** ni kati ya asilimia **89.05** hadi **97.88**. Aidha, ufaulu wa masomo yote ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umepanda kwa kati ya asilimia **0.12** na **30.66** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2023. Somo la **Theatre Arts** limeongeza ufaulu kwa kiwango kikubwa **(30.66%)** likifuatiwa na somo la **Physical Education** lililoongeza ufaulu kwa asilimia **8.29**. Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo yana ubora wa ufaulu wa kati ya asilimia **51.67** na **84.21**. Aidha, masomo yote yameongeza ubora wa ufaulu kwa kati ya asilimia **0.26** na **24.77**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 8**.

**Jedwali Na. 8: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fine Art | 2023 | 1,072 | 5.13 | 18.84 | 65.11 | 97.76 | 2.24 |
| | 2024 | 1,793 | 3.35 | 11.66 | 65.37 | 97.88 | 2.12 |
| Music | 2023 | 36 | 0.00 | 16.67 | 72.22 | 94.44 | 5.56 |
| | 2024 | 57 | 45.61 | 66.67 | 84.21 | 94.74 | 5.26 |
| Physical Education | 2023 | 2,039 | 0.05 | 1.23 | 45.51 | 87.40 | 12.60 |
| | 2024 | 1,833 | 1.09 | 7.58 | 66.72 | 95.69 | 4.31 |
| Theatre Arts | 2023 | 435 | 0.00 | 1.15 | 26.90 | 58.39 | 41.61 |
| | 2024 | 420 | 6.19 | 16.43 | 51.67 | 89.05 | 10.95 |

### 3.4.6 Masomo ya Ufundi

Ufaulu wa jumla wa masomo yote ya ufundi ni mzuri ambao ni kati ya asilimia **86.30** na **100**. Aidha, Ubora wa ufaulu kwa masomo hayo ni kati ya asilimia **54.55** na **95.03** isipokuwa somo la **Civil Engineering Surveying** lenye ubora wa ufaulu wa asilimia **29.68**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Ufundi umeoneshwa katika **Jedwali Na. 9**.

**Jedwali Na. 9: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Ufundi**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Building Construction | 2023 | 398 | 1.01 | 7.79 | 70.10 | 92.96 | 7.04 |
| | 2024 | 398 | 3.02 | 17.84 | 81.91 | 98.24 | 1.76 |
| Architectural Draughting | 2023 | 363 | 0.00 | 3.31 | 41.05 | 92.01 | 7.99 |
| | 2024 | 390 | 3.33 | 15.13 | 79.23 | 97.95 | 2.05 |
| Civil Engineering Surveying | 2023 | 133 | 0.00 | 2.26 | 41.35 | 84.96 | 15.04 |
| | 2024 | 219 | 0.00 | 1.83 | 29.68 | 86.30 | 13.70 |
| Woodwork and Painting Engineering | 2023 | 187 | 0.00 | 0.00 | 36.36 | 88.24 | 11.76 |
| | 2024 | 131 | 0.76 | 6.11 | 74.81 | 96.18 | 3.82 |
| Electrical Engineering | 2023 | 320 | 6.88 | 21.56 | 71.56 | 93.13 | 6.88 |
| | 2024 | 331 | 7.85 | 24.47 | 72.51 | 90.94 | 9.06 |
| Electronics and Communications Engineering | 2023 | 215 | 0.47 | 5.58 | 53.49 | 91.16 | 8.84 |
| | 2024 | 275 | 0.73 | 9.45 | 54.55 | 92.00 | 8.00 |
| Electrical Draughting | 2023 | 247 | 3.24 | 12.15 | 49.39 | 87.04 | 12.96 |
| | 2024 | 260 | 10.77 | 27.69 | 65.77 | 91.92 | 8.08 |
| Electronics Draughting | 2023 | 197 | 3.05 | 20.81 | 77.16 | 97.46 | 2.54 |
| | 2024 | 234 | 3.85 | 16.24 | 65.81 | 94.87 | 5.13 |
| Automotive Engineering | 2023 | 183 | 3.83 | 22.95 | 84.70 | 96.72 | 3.28 |
| | 2024 | 169 | 22.49 | 50.89 | 93.49 | 100 | 0.00 |
| Manufacturing Engineering | 2023 | 133 | 9.02 | 27.82 | 78.20 | 93.23 | 6.77 |
| | 2024 | 188 | 18.09 | 39.36 | 80.85 | 96.81 | 3.19 |
| Engineering Drawing | 2023 | 231 | 3.46 | 16.88 | 58.87 | 88.74 | 11.26 |
| | 2024 | 318 | 2.52 | 16.35 | 68.24 | 94.65 | 5.35 |
| Textile and Garment Construction | 2023 | 143 | 12.59 | 30.77 | 90.21 | 100 | 0.00 |
| | 2024 | 181 | 6.63 | 31.49 | 95.03 | 100 | 0.00 |

### 3.4.7 Masomo ya Dini

Watahiniwa waliofaulu somo la **Bible Knowledge** ni asilimia **99.08** na katika somo la **Elimu ya Dini ya Kiislamu** ni asilimia **79.83**. Ufaulu wa somo la **Bible Knowledge** umepanda kwa asilimia **0.43** na katika somo la **Elimu ya Dini ya Kiislamu** ufaulu umeshuka kwa asilimia **1.99** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka

2023. Watahiniwa waliopata ufaulu wa kati ya gredi **A** hadi **C** katika somo la **Bible Knowledge** ni asilimia **96.69** na katika somo la **Elimu ya Dini ya Kiislamu** ni asilimia **35.22**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Dini umeoneshwa katika **Jedwali Na. 10**.

**Jedwali Na. 10: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Dini**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bible Knowledge | 2023 | 16,064 | 53.37 | 80.98 | 96.40 | 98.65 | 1.35 |
| | 2024 | 15,703 | 38.75 | 74.39 | 96.69 | 99.08 | 0.92 |
| Elimu ya Dini ya Kiislamu | 2023 | 80,638 | 2.24 | 11.38 | 52.04 | 81.82 | 18.18 |
| | 2024 | 84,023 | 0.71 | 3.51 | 35.22 | 79.83 | 20.17 |

## 4.0 MATOKEO YALIYOZUILIWA

Baraza la Mitihani la Tanzania **limezuia** kutoa matokeo ya watahiniwa **459** ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne, 2024 kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo. Watahiniwa husika wamepewa fursa ya kufanya Mtihani kwa masomo ambayo hawakuyafanya kwa sababu ya ugonjwa mwaka 2025 kwa mujibu wa Kifungu cha **32**(**1**) cha Kanuni za Mitihani.

## 5.0 MATOKEO YALIYOFUTWA

Baraza la Mitihani **limefuta** matokeo yote ya watahiniwa **67** waliobainika kufanya udanganyifu na watahiniwa **05** walioandika lugha ya matusi katika skripti zao katika Mtihani wa Kidato cha Nne.

Matokeo hayo yamefutwa kwa mujibu wa Kifungu cha **5 (2) (j)** cha Sheria ya Baraza la Mitihani sura ya **107** kikisomwa pamoja na Kifungu cha **30(2) (b)** cha Kanuni za Mitihani Mwaka **2016**.

## 6.0 KITUO KILICHOFUNGIWA KUWA KITUO CHA MITIHANI YA TAIFA

Baraza la Mitihani la Tanzania limefungia kituo cha **P6384 BSL Open School** kilichopo mkoa wa **Shinyanga** kuwa kituo cha Mitihani ya Taifa kutokana na kuratibu mipango ya udanganyifu. Kituo hicho kinafungiwa kwa mujibu wa

Kifungu **4**(**8**) cha Kanuni za Mitihani mwaka 2016 hadi hapo Baraza litakapojiridhisha kuwa ni salama kwa uendeshaji wa Mitihani ya Taifa.

## 7.0 PONGEZI ZA BARAZA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati za Uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/Manispaa/Jiji, Wakuu wa Shule, Wasimamizi na Wasahihishaji wa Mtihani wa Kidato cha Nne, uliofanyika Novemba, 2024 kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika kutekeleza jukumu la Uendeshaji Mtihani huo. Aidha, Baraza linawapongeza watahiniwa wote waliofanya Mtihani kwa kuwa na utulivu na kuzingatia taratibu za mitihani katika kipindi chote cha Uendeshaji wa Mitihani.

## 8.0 UPATIKANAJI WA MATOKEO

Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne, 2024 uliofanyika Novemba, 2024 yanapatikana katika tovuti zifuatazo:

- www.necta.go.tz,
- www.moe.go.tz,
- www.tamisemi.go.tz.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**
**23/01/2025**